

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**



**MWONGOZO WA KUPIMA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA(COVID-19)**  
**KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA**

**UTANGULIZI**

Kulingana na mwenendo wa sasa wa Mlipuko wa Ugonjwa wa COVID-19 nchini, Wizara imeandaa utaratibu na vigezo vya watu wanaostahili kuchukuliwa sampuli ili kupima COVID-19. Watakaokidhi vigezo vifuatavyo wanakidhi vigezo vya kuchukuliwa sampuli kwa ajili ya vipimo vya COVID-19.

**VIGEZO VYA KUCHUKULIWA SAMPULI.**

1. Wahisiwa wa Ugonjwa wa COVID-19, waliokidhi vigezo vya kuwa na viashiria vya ugonjwa (**Standard case definition**).
2. Wenye dalili za wastani au kali (Moderate, severe or critical symptoms) za ugonjwa wanaohisiwa kuwa na maambukizi ya COVID-19 kama (Homa, kupumua kwa shida).
3. Wenye magonjwa sugu na magonjwa yasiyoambukiza wanapojisikia vibaya au vipimo vya magonjwa muda mrefu/sugu kuanza kupanda juu kama Sukari au BP, au kuchoka sana bila sababu ya msingi.
4. Upimaji wa Makundi maalumu
  - a. Madereva wa Magari ya Mizigo wanaoingia na kutoka ndani ya nchi.
  - b. Wasafiri wa ndege wanaoingia au kutoka nchini kwa sababu maalumu.

Utaratibu huu utaendelea kufuatwa mpaka hapo Wizara itakapotoa utaratibu mwingine. Waganga wakuu wa Mikoa, Wilaya, Hospitali za rufaa za Kanda na Taifa na Waganga wafawidhi wa Hospitali zote nchini, za umma na binafsi wanaagizwa kusimamia utekelezaji wa utaratibu huu.

  
Prof. Abel N. Makubi  
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**